


DeKalb County School District

## Maswali Yanayoulizwa Sana – Familia

*Maswali Yanayoulizwa Sana*

**Je, ninaweza kupata wapi ratiba ya sherehe ya mahafali ya Wilaya?** Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb itaandaa sherehe 23 kati ya 24 za mahafali tarehe 11 hadi 19 Mei 2024 katika GA State Convocation Center iliyoko Georgia State Convocation Center, 455 Capitol Avenue, SE, Atlanta, GA 30312. Shule ya Margaret Harris Comprehensive itaandaa sherehe yake ya mahafali katika siku ya Ijumaa, tarehe 10 Mei 2024 shuleni mwao. Ratiba ya sherehe za mahafali imewekwa kwenye tovuti ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb. Unaweza kutembelea tovuti hii kwa kutumia kiungo kifuatacho: https://www.dekalbschoolsga.org/graduation

**Je, usafiri utatolewa kwa wanafunzi?** Ndiyo. Mabasi yaliyokodishwa yenye viyoyozi yatatolewa kwa shule zote kwa ajili ya safari za kwenda na kurudi kutoka GA State Convocation Center. **Hakuna ada kwa wanafunzi kupanda mabasi yaliyokodishwa.** Walimu wakuu watampa kila mhitimu Fomu ya Ruhusa ya Usafiri ili wazazi waijaze na kuirudisha ikionyesha ikiwa mwanafunzi wao atasafiri kwa basi lililokodishwa kwenda na kutoka GA State Convocation Center. Walimu wakuu watatoa taarifa za saa za kuchukuliwa na kurudishwa kwa wazazi/wahitimu. Wasindikizaji wa shule watasafiri kwenye mabasi pamoja na wahitimu.

**Je, wahitimu wanapaswa kufika katika GA State Convocation Center saa ngapi?** Wahitimu watasafirishwa hadi Convocation Center saa moja kabla ya wakati ulioratibiwa wa kuanza kwa sherehe yao kwa ajili ya maandalizi ya sherehe ya mahafali. Mabasi yaliyokodishwa yatawasafirisha wanafunzi kurudi shuleni mara baada ya kumalizika kwa sherehe yao.

**Je, wazazi/wanafamilia wanapaswa kufika saa ngapi kwenye sherehe ya mahafali ya mwanafunzi wao?** Maeneo ya maegesho katika GA State Convocation Center yatafunguliwa saa moja kabla ya wakati ulioratibiwa wa kuanza kwa kila sherehe ya mahafali. **Wageni wanaohudhuria sherehe wataingilia na kuondoka kupitia vibanda vya tiketi pekee -- vilivyopo katika Capitol Avenue (*ANGALIA RAMANI ILIYOAMBATISHWA*)**.. *Tafadhali tumia ramani iliyoambatishwa ya Convocation Center ili kupanga safari yako.*

**Je, nitahitajika kulipia maegesho?** Hutalipishwa ada ya maegesho ikiwa ***utatumia maeneo yaliyotajwa hapa chini*** katika tarehe mahususi zilizotajwa.

**Mei 11** – Bluu, Kijani, Summerhill B na C

**Mei 14** – Bluu, Kijani, Summerhill C

**Mei 15** – Bluu, Kijani, Summerhill C

**Mei 16** – Bluu, Kijani, Summerhill C

**Mei 19** – Bluu, Kijani, Summerhill B na C

**MAEGESHO YA WALEMAVU**

*Yanapatikana Katika Kila Eneo la Maegesho*

HATA HIVYO, USAIDIZI WA KIGARI CHA GOFU UNAPATIKANA

**TU** KATIKA MAENEO YAFUATAYO YA MAEGESHO:

**1) ENEO LA BLUU**

**2) ENEO LA SUMMERHILL C**

**Je, ninahitajika kuwa na tiketi ili kuingia kwenye sherehe ya mahafali? Je, kuna viti vilivyotengwa kwenye sherehe ya mahafali?** Ndiyo, unahitaji kuwa na tiketi ili kuingia kwenye sherehe za mahafali. Viti vimetengwa kwa wageni wa wahitimu wanaoshikilia nafasi ya kwanza na ya pili. Unaweza kukosa kiti ikiwa utachelewa kufika GA State Convocation Center.

**Je, nitakutana wapi na mwanafunzi wangu baada ya sherehe ya mahafali kukamilika?** Wahitimu wataondoka kwenye GA State Convocation Center ili kuondoka kwenye kituo. Wageni wakiwa wamepanga foleni wataondoka kupitia vibanda vya tiketi. Ikiwa mwanafunzi wako anapanga kupanda basi lililokodishwa ili kurudi kwenye shule yake ya upili, ataenda moja kwa moja kwenye basi ili kuondoka mara moja kwenye kituo baada ya sherehe. Ikiwa mhitimu wako amepanga kusafiri nawe kwenda nyumbani, tafadhali mwambie akutane nawe katika kiingilio cha wageni kwenye Capitol Avenue na mpange ipasavyo mapema **(Angalia Ramani Iliyoambatishwa).**




# Maswali Yanayoulizwa Sana-Familia yanaendelezwa

*Maswali Yanayoulizwa Sana*

**Wahitimu watapokea diploma zao lini?**
Wahitimu watapata folda za kuweka diploma wakati wa sherehe. Kila shule ya upili imetenga tarehe na wakati ambao wahitimu watachukua diploma zao shuleni mwao. Shule zitatoa taarifa za ziada kabla ya sherehe.

**Je, nitapata fursa ya kupiga picha za mhitimu wangu jukwaani?**
Hapana. Mpiga picha aliyeajiriwa atachukua mfululizo wa picha za kila mhitimu ili kuadhimisha tukio hili maalum. Wahitimu watapata picha yao wakipokea folda zao za kuweka diploma jukwaani kama sehemu ya kifurushi chao cha kuhitimu. Mpiga picha atashiriki picha za ziada za wahitimu na shule/wahitimu ambazo zitapatikana kwa ununuzi.

**Mhitimu wangu anahitajika kuleta nini kwenye sherehe ya mahafali?**
Wahitimu na wageni wanapaswa kuvaa viatu vinavyowatoshea vizuri na wabebe mikoba michache. Wilaya itaandaa sherehe nne hadi tano za mahafali kila siku. Chumba cha mazoezi ya wahitimu katika kituo kinapaswa kuondolewa vitu na kusafishwa mara baada ya wahudhuriaji kuondoka eneo hilo ili kuandaliwa kwa sherehe inayofuata. Wahitimu wanapaswa kuingia kwenye ukumbi wa sherehe bila vifaa visivyoidhinishwa na wilaya kama vile medali, kamba za heshima, riboni n.k. Wahitimu wanapaswa kuvaa viatu vinavyowatoshea ndani ya ukumbi kwa sababu za usalama. Wahudhuriaji wanaruhusiwa tu kuleta mikoba inayoonekana ndani kwenye kituo.

**Je, chakula kinaruhusiwa katika sherehe ya kuhitimu?**
Hapana. Chakula hakiruhusiwi uwanjani. Wahitimu na wageni wanaombwa kula kabla ya sherehe yao ya mahafali. Wahitimu na wageni wanaombwa pia kuhakikisha wanakunywa maji ya kutosha wanapohudhuria sherehe.

**Je, sherehe za mahafali zinarekodiwa?**
Ndiyo. Kila sherehe ya mahafali itarekodiwa na kutangazwa kupitia kiungo cha mtiririko wa moja kwa moja. Viungo vya kutazama sherehe vitatolewa kwenye tovuti ya Grad Central Station: https://www.dekalbschoolsga.org/graduation/ Kuwa uwezekano kwamba wahudhuriaji wanaweza kupigwa picha, kurekodiwa video au picha wakati wa kupiga picha au kurekodi sherehe hizi. Wahitimu wanaweza kupakua nakala za sherehe zao kupitia YouTube.

**Ni taarifa gani za ziada unaweza kushiriki nami ninapopanga ziara yangu?**

- Kupanga mapema ili kuwasili mapema ni muhimu. *Tafadhali tumia ramani iliyoambatishwa kupanga safari yako.*
- **Tarajia kutembea kwa umbali mrefu kutoka eneo la maegesho -- vaa viatu vinavyokutoshea.**
- **Maeneo ya kuketi katika uwanjani yameinama sana. Tafadhali kuwa mwangalifu.**
- Simu za mkononi/vifaa vyote vya kielektroniki lazima viwekwe katika hali kimya kabla ya kuingia kwenye uwanja.
- **Puto, vitoa kelele, ishara, mizigo, mifuko ya mgongoni n.k**. hazikubaliwi katika uwanja. ***Tafadhali angalia kipeperushi kilichoambatishwa***.
- Wageni wanaohudhuria sherehe wataingilia na kuondoka kupitia vibanda vya tiketi vilivyoko Capitol Avenue.
- Viti vya magurudumu vinapatikana kwa wahudhuriaji ambao wanaweza kuvihitaji kwenye uwanja. Wahudhuriaji walio na uwezo mdogo wa kutembea ambao hawahitaji usaidizi wa viti vya magurudumu wanaweza kuingia kwenye uwanja na kuketi kwenye viti vya chini zaidi.
- Wageni wa wanafunzi wanaoshikilia nafasi za kwanza na pili wataketi karibu na ngazi ya chini zaidi karibu na wahitimu.
- Wageni wanafaa kuingia uwanjani na mikoba inayoonekana ndani pekee. Panga ipasavyo kwa hali mbaya ya hewa.
- Viti ni vichache. **Usisahau kubeba tiketi yako. Unahitaji** kuwa na tiketi ili kuingia uwanjani.
- UJUMBE WA DHARURA KWA WAHITIMU NA WAGENI: Wahudhuriaji wote watahitajika kupekuliwa kwa kutumia Vifaa vya Utambuzi wa Silaha.










**Sera ya Mikoba Inayoonekana Ndani**

Wageni wanahitajika kubeba mikoba inayoonekana ndani na kushika mikoba yao ambayo haizidi ukubwa wa inchi 12” X 6” X 12”, mifuko ya plastiki ya friza yenye ukubwa wa galoni 1, na/au mkoba wa kushika kwa mkono usiozidi inchi 4.5” X 6.5”, takriban ukubwa wa mkono.

Mikoba inayozidi inchi 12” X 6” X 12” na mifuko ya mgongoni haikubaliki katika GSU Convocation Center. Mikoba mikubwa inaweza kukubalika kwa watu walio na mahitaji ya kubeba dawa, nepi na mahitaji maalum.

Mikoba yote lazima ipekuliwe. Wageni wanahimizwa warudishe mikoba isiyokubalika kwenye magari yao. Georgia State University HAITATOA kituo cha kupekua mikoba ambacho ni salama na kinachofuatiliwa ili kuruhusu wageni kupekuliwa mikoba wanapoingia na kuondoka kwenye hafla.

Wahudhuriaji wataingia kupitia vifaa vya kutambua silaha.

Marekebisho kulingana na Sheria ya Wamarekani walio na Ulemavu (ADA):

Viti kulingana na sheria ya ADA vinapatikana katika upande wa **juu wa sehemu katika kiwango cha 100.** Kutoka kwa plaza na makutano hakuna ngazi kwenye njia inayoelekea kwenye viti hivi. **Viti na maegesho kulingana na sheria ya ADA ni machache na yatapatikana kwa misingi ya wale watakaofika mapema.**

**Vitu Visivyoruhusiwa:** Kwa ajili ya usalama wa wahudhuriaji, vitu na shughuli zifuatazo haziruhusiwi katika Convocation Center:

**Vipaza sauti bandia, wanyama, mifuko ya mgongoni, vyakula na vinywaji vya nje, fataki, puto, baiskeli, bao za kuteleza, skuta na viatu vya kusketi, vipozaji, vitu visivyo halali, viashiria vya leza, nguzo za bendera na vijiti, vitembezi kwenye viti, kamera za video, silaha, alama kubwa.** Unapaswa kuweka simu za mkononi/vifaa vyote vya kielektroniki katika haki kimya kabla ya kuingia uwanjani

# GEORGIA STATE CONVOCATION CENTER
455 CAPITOL AVENUE, SE
ATLANTA, GA 30312

*Tafadhali Kumbuka*:

**Maegesho hayalipishwi. Tutatumia maegesho yafuatayo kwa kila siku:**

**Mei 11** – Bluu, Kijani, Summerhill B na C
**Mei 14** – Bluu, Kijani, Summerhill C
**Mei 15** – Bluu, Kijani, Summerhill C
**Mei 16** – Bluu, Kijani, Summerhill C
**Mei 19** – Bluu, Kijani, Summerhill B na C

## MAEGESHO YA WALEMAVU

*Yanapatikana Katika Kila Eneo la Maegesho*

HATA HIVYO, USAIDIZI WA KIGARI CHA GOFU UNAPATIKANA KATIKA MAENEO YAFUATAYO YA MAEGESHO:

1) **MAEGESHO YA BLUU**
2) **MAEGESHO YA SUMMERHILL C**

## MARTA

Kituo cha karibu zaidi cha Marta ni kituo cha Georgia State Station katika 170 Piedmont Ave SE, Atlanta, GA 30303, takriban maili .7 kutoka Convocation Center.

